HALMASHAURI YA WILAYA YA TUNDURU

MKUU WA SHULE - 0753412885
MAKAMU M/SHULE - 0782062701
Kumb.Na.MGSS/JI/VOL.1/20

SHULE YA SEKONDARI MGOMBA
S.L.P 460
TUNDURU
11/12/2020

JINA LA MWNAFUNZI ……..
S.L.P ……..
TUNDURU

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MGOMBA –WILAYA YA TUNDURU, MKOA WA RUVUMA MWAKA 2021

1.0 UTANGULIZI

Nina furaha kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2021. Shule ya sekondari Mgomba ipo magharibi ya mji wa Tunduru. Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe 11/01/2021, hivyo unatakiwa kuripoti tarehe hiyo bila kukosa.

2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

2.1 SARE ZA SHULE

(A) WASICHANA

i) Sketi (2) rangi kijani kibichi kilichoiva zilizopita magoti za heshima zisizobana zenye mtindo wa rinda box (vitambaa vipo maduka ya nguo)
ii) Mashati meupe mikono mifupi ya saizi yako
iii) Viatu vya ngozi vyeusi vya kamba (gidamu) visiwe na kisigino kirefu jozi 2.
iv) Soksi nyeupe jozi 2
v) Sweta la kijani

NB: Wasichana wanaruhusiwa kushona hijabu ambayo inatakiwa ifanane na sare ya shule. Hijabu inatakiwa kuwa na nusu kanzu, isiyobana na kitambaa aina ya koshibo.

(B) WAVULANA

i) Suluali 2 za heshima zisizo na mtindo. Rangi ya kitambaa kijani kibichi (maduka ya nguo kinapatikana)
ii) Mashati meupe mikono mifupi 2
iii) Viatu vyeusi vya ngozi vya kamba (giamu) jozi 2
iv) Sosi nyeusi ndefu jozi 2
v) Mkanda mweusi
vi) Sweta la kijani

NB: Hakikisha suluali yako mkanda unafunga kiunoni na siyo kwenye makalio

(C) SARE YA MICHEZO

WASICHANA

i) Viatu raba yeusi jozi 1
ii) Track suit za bluu jozi 1

WAVULANA

i) Viatu raba nyeusi jozi 1
ii) Bukta 2 za bluu
iii) T-shirt 2 za bluu zisizo na maandishi

2.2 VIFAA VYA DARASANI

i) Daftari za kaunta (quire 2) 10
ii) Mkebe (mathematical set) 1
iii) Kalamu za wino 10
iv) Penseli 2
v) School bag 1
vi) Mwamvuli au koti la mvua 1

2.3 VIFAA VYA USAFI NA CHAKULA

i) Ndoo ndogo 1 } **wote**
ii) Bakiuli, sahani, kikombe na kijiko
iii) Reki }
iv) Fyekeo } **wasichana**
v) Panga }
vi) Jembe lenye mpini } **wavulana**

2.4 MCHANGO WA CHAKULA

Lete mahitaji yafuatayo kwa ajili ya chakula cha mchana kwa muhula (januari-juni 2021) (kamati ya wazazi ya chakula ndiyo inayoshughulikia)

MAHINDI	MAHARAGE	CHUMVI	MAFUTA YA KULA	KUSAGA NA MPISHI	KUNI
40KGS	7.5 KGS	2 KGS	2 LITA	5,600/=	3/WIKI

3.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yenye dhamana ya Elimu Nchini.

UNATAKIWA KUZINGATIA MAMBO YA MSINGI YAFUATAYO

a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni muhimu
c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio uya jioni (preparation)
d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako shule hii.
f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingiraa ya shule
g) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
h) Kutunza mali za uma

3.1 MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE

a) Wizi
b) Uasherati na ushoga
c) Ubakaji
d) Ulevi na matumizi ya dawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cpcaine, mirungi, kubeli, na kadhalika.
e) Kupigana au kupiga
f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
g) Kudhalau bendera ya taifa
h) Kuwa mjamzito/ kupata mimba
i) Kuoa au kuolewa
j) Kutoa mimba
k) Kugoma, kuchochea, na kuongoza na kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
l) Kukataa adhabu kwa maksudi
m) Kuwa na simu ya mkononi

4.0 MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI

a) Medical examination form, ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali. Fomu hii itakakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara atakaporipoti shuleni.
b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanfunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
c) Fomu ya mzazi kukubaliana naa sheraia, kanuni na maelezo mengine yatakayotolewa na shule

5.0 Tafadhali somo kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBUNI SANA KATIKA SHULE HII
MOTTO WA SHULE- MAARIFA HUJENGA UWEZO (KNOWLEDGE IS POWER)



NIVER .R.MBUNDA
MKUU WA SHULE

HALMASHAURI YA WILAYA YA TUNDURU
SHULE YA SEKONDARI MGOMBA

S.L.P 460
TUNDURU
11/12/2021

FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MGOMBA
MWANAFUNZI

1. Mimi …….. ninakubali/ sikubali kujiunga kidato cha kwanza katika shule ya sekondari ya kutwa ya Mgomba.
2. Ninahaidi kufika shuleni tarehe 11/01/2021 iliyopangwa bila kuchelewa.
3. Ninahaidi kwamba nitakuwa mwanafunzi mwenye bidii na utii kwa sheria za shule, walimu, watumishi wasio watumishi, wanafunzi viongozi, wanafunzi wanajumuia wa ndani na nje ya shule muda wote.
4. Kamwe sitakuwa mtoro wa shule pia sitoshiriki kwa namna yeyote katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
   SAINI YA MWANAFUNZI ……..
   TAREHE ……

MZAZI/MLEZI

1. Mimi ……... nimekubali/ sijskubali mtoto wangu kujiunga na shule ya sekondari mgomba
2. Ninahaidi kuwa mtoto wangu ataripoti shuleni bila kuchelewa kama vilivyo tajwa kwenye barua ya maagizo (joining instruction)
3. Nitahakikisha ya kwamba mtoto wangu amesoma vizuri sheria za shule na kuzielewa na nitamtaka azitekeleze sheria izo kwa vitendo.
4. Nitashirkiana na uongozi wa shule na mamlaka zingine kupiga vita aina zote za utovu wa nidhamu iikiwemo utoro, migomo fujo na makosa ya jinai.
5. Ninhaidi kufuatilia kwa karibu maendeleo ya mtoto kimasomo na kitabii
   Anwani yangu
   a) Mtaa/kijiji ……
   b) Kata …….
   c) Tarafa …….
   d) Saini ya mzazi/mlezi …… Tarehe …….
   e) Simu ……

AHSANTE

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI MGOMBA
P.O.BOX 460–TUNDURU

NIVER .R. MBUNDA
MKUU WA SHULE

OR-TAMISEMI

RUVUMA REGION
MOBILE NO.

MGOMBA SECONDARY SCHOOL
P.O.BOX 460
TUNDURU
DATE …….

TO THE MEDICAL OFFICER
……
……
……

REF: REQUEST FOR MEDICAL EXAMINAATION
PLEASE EXAMINE A STUDENT (FULL NAME)
…… age ……... sex …… so as to join secondary school education.

GENERAL CONDITION OF HEALTH
HEAD:
Eyes
……
Ears
……
Mouth …….
Nose ……

CHEST X-RAY REPORT
Heart ……..
Abdomen …….
Extreme Ties …….

LAB. FINDINGS
Blood group ……
Stool ……
Urine …….
H.B ……..
Lanceted …….
ESR …….
Pregnancy …….
Others ……
MEDICAL CERTIFICATION
I have examined that above named and consider that he or she is fit or unfit to join school

…… ……. ……..
DATE SIGNATURE DESIGNATION